# ...a mzaha na Corona


...biashara kutowahudumia
...asiovaa barakoa, kinyume
...o ni kukiuka maagizo ya

...mshukuru Rais John
...li kwa kuendelea
...za Watanzania, kujihdhari
...da kwa kutumia vifaa
...ani bila wananchi kuwa
...bora, hakuna shughuli
...leleo na hivyo viongozi
...na na wananchi tuwe na
...a watu wetu wanyonge,
...atuwezi kuwa viongozi,"
...winyikondo.
...huyo alitumia fursa hiyo
...arakoa kwa baadhi
...chi wa mitaa nane
...hiyo, wakiwemo
...a pikipiki na kuwashauri
...awaelimisha abiria wao
...e Sanitizer kuwakinga
...a.
...ande wake Mwenyeviti
...a Kiseke, Juma Msaka

waliwataka wananchi wa mitaa hiyo na mingine kufuata maelekezo ya wataalamu wa afya na serikali, ili kuwa salama na familia zao na watutumie vitakasa mikono, wavae barakoa na kunawa mikono bila shuruti, kufanya hayo itakuwa ni kuiunga mkono serikali.

Naye Mwenyekiti wa Mtaa wa Kabambo, Maulid Ahungu aliwahimiza wazazi kuwalinda na kutofawafanyisha watoto biashara, au kwenda kwenye mikusanyiko kipindi hiki cha ugonjwa wa Corona.

Mkazi wa Mtaa wa Greenview, Majaliwa Hagai alisema awali alikuwa akipuuza na wananchi wengi walikuwa wanadharau kuhusu ugonjwa wa Corona, lakini kutokna na vifo vinavyotokea, amebaini ugonjwa huo si wa mzaha na kuwasihi wananchi wengine kuchukua tahadhari na kuacha mzaha.



...pofanya ziara Wilaya ya Kigamboni jana kukagua
(...ha Wetu)

# ...izi mazuri ya fedha

...kujikinga na ugonjwa
...pa na kuwepo kwa
...a kuwawezesha
...chumi pindi ugonjwa
...sha nchini kutokana
...kuyumba mitaji huku
...opo katika taasisi za

...iamali, Bumi Juma
...mba serikali kufanya
...ekana kufunguliwe
...shule kwani tangu
...a uchumi imeyumba
... watoto kujiingiza
... ambayo ni hatarishi
...kukosa usimamizi
...azi katika ngazi ya

...zifungwe kwa kweli

akinamama wamekuwa na mzigo mkubwa wa kutunza familia na hata kushindwa kuwasimamia, jambo ambalo linasababisha kujihusisha katika michezo isiyofaa ikiwa ni pamoja na ajira za utotoni na michezo ya kubahatisha," alisema.

Kwa upande wake Mkazi wa Forest jijini hapa, Athanas Mhagama alisema licha ya kuyumba kwa uchumi lakini jamii bado inapaswa kutumia elimu inayotolewa na wataalamu katika kujikinga na ugonjwa wa Corona, sambamba na kuwepo kwa vifaa maalumu vya kupima joto katika taasisi mbalimbali za serikali na karantini za kuwahifadhi wagonjwa wanaokutwa na dalili kwenye maeneo ya vijijini.

MAJIRA UK 10.

# Upatikanaji wa maji kumaliza ugomvi wakulima, wafugaji

**Na Omary Mngindo, Mlandizi**

WAKAZI wa vijiji na vitongoji vinavyounda Kata ya Magindu Kibaha Vijijini Mkoa wa Pwani, wameanza kunufaika na huduma ya maji safi na salama katika maeneo yao.

Hatua hiyo huenda ikawa tiba ya tatizo sugu la ugomvi kati ya wakulima na wafugaji, ambapo mwaka lilisababisha kifo cha mkulima aliyeuawa kwa mkuki Machi 26 2019, kutokana na kugombea lambo lenye maji, hali iliyofanya mkazi huyo kuchomwa mkuki na kupoteza maisha.

Hayo yalielezwa na Diwani wa Kata hiyo, Mohamed Mkali mbele ya Baraza la Madiwani wa halmashauri chini ya Mwenyekiti Mansour Kisebengo, Makamu Mwajuma Denge na Mkurugenzi Butamo Ndalahwa ambapo, Mkali alielezea furaha hiyo.

Alisema baada ya adha ya muda mrefu kwa wakazi katika kata hiyo kuhangaika kutafuta maji, hatimaye DAWASA ambayo awali ilijulikana kama CHALIWASA imefanikisha kuondoa tatizo hilo, hivyo kwenda kupunguza kama si kumaliza migogoro ambayo chanzo kikubwa ni maji.

"Mheshimiwa Mwenyekiti, ninayo furaha ya kuliarifu baraza lako kwamba hivi sasa huduma ya maji imeanza kupatikana katika baadhi ya vijiji na vitongoji vinavyounda Kata yangu ya Magindu, nitumie fursa hii kuishukuru serikali inayoongozwa na Rais John Magufuli kwa kazi inayoendelea kutekelezwa," alisema Mkali.

Akizungumza kwenye baraza hilo, Kisebengo alielezea furaha yake kutokana na taarifa hiyo njema kwa wakazi wa Magindu, huku akisema kwa muda mrefu walikuwa katika changamoto kubwa ya upatikanaji wa huduma hiyo muhimu.

"Tunaishukuru serikali yetu chini ya rais, anayesikiliza na kuzifanyiakazi changamoto za wananchi wake, suala la maji katika maeneo ya Magindu na vitingoji vyake limeendelea kufanyiwa kazi na sasa Diwani Mkali ametujulisha kupatikana kwa huduma hiyo," alisema.

Kwa upande wake Mkurugenzi, Ndalahwa aliwataka watendaji wote kuhakikisha wanawasilisha fedha zinazotokana na makusanyo ya tozo mbalimbali na kwamba kukaa nazo pasipokuziweka benki ni kinyume cha sheria.

"Kuanzia sasa watendaji ambao hawajawasilisha fedha za makusanyo benki wafanye hivyo haraka, kitendo cha kukaa nazo pasipokuwa na taarifa ni kinyume cha sheria," alisema Ndalahwa.

Scanned with CamScanner